

**HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA  
YA HALI YA HEWA, DKT. AGNES KIJAZI,  
KWENYE UFUNGUZI WA WARSHA INAYOHUSU  
KUONGEZA UFAHAMU KWA WAFANYAKAZI WA  
MAMLAKA KUHUSU MPANGO MKAKATI WA  
MIAKA MITANO (2016/17-2020/21) WA  
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA, KATIKA  
UKUMBI WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA,  
MAKAO MAKUU JENGO LA UBUNGO PLAZA,  
GHOROFA YA 3, DAR ES SALAAM; TAREHE 29  
SEPTEMBER 2017.**

**Ndugu Wakurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa  
Tanzania;**

**Mameneja;**

**Wataalamu kutoka vitengo mbalimbali vya Mamlaka;**

**Ndugu Wanawarsha;**

**Mabibi na Mabwana,**

Ninayo furaha kujumuika nanyi leo kwenye warsha hii muhimu yenye lengo la kuongeza ufahamu (awareness raising) kwa wafanyakazi wa Mamlaka kuhusu Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (**TMA Strategic Plan 2016/17-2020/21**) na kuweka maazimio ya utekelezaji wake. Warsha hii ni mwendelezo wa vikao vya wadau vilivyolenga kupata maoni ya namna ya utekelezaji wa Mpango Mkakati huu. Kwa kuwa mpango huu ni wa Mamlaka, tumeona ni vema kukaa na wadau wa ndani ili kupata kuufahamu vyema ambapo itachangia utekelezaji wake. Maandalizi ya Mpango huu yalifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) kupitia Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa niaba yangu binafsi napenda kuendelea kutoa shukrani zangu za dhati kwa

Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) kwa kufadhili uandaaji wa mpango huu ikiwa ni pamoja na warsha hii ya leo. Shirika la Hali ya Hewa Ulimwenguni limeendelea kufanya kazi kubwa ya kuimarisha huduma za hali ya hewa duniani na kusaidia nchi za Afrika katika kuboresha huduma za hali ya hewa.

### **Ndugu Wanawarsha, Mabibi na Mabwana,**

Mpango Mkakati huu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) unaoanzia mwaka huu wa 2017 hadi 2021 ni mwongozo muhimu kwa TMA na wadau katika kuhakikisha kuwa masuala ya hali ya hewa yanaendelea kuingizwa na kuwa sehemu ya mipango ya maendeleo ya Taifa katika kipindi hicho cha miaka mitano. Aidha unatoa mwongozo na kuweka vipaumbele ambavyo vitasaidia kutoa

maamuzi katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Mpango huu unazingatia ukuaji wa huduma bora za hali ya hewa na zinazopatikana kwa wakati na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi wetu na kusaidia kuokoa maisha ya watu na mali zao kutokana na hali mbaya ya hewa.

### **Ndugu Wanawarsha, Mabibi na Mabwana,**

Ikumbukwe kwamba, Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika zinazoendelea kuathiriwa au zilizo katika hatari ya kukumbwa na majanga ya hali ya hewa hususan yale yanayosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Matukio ya mara kwa mara ya mafuriko na ukame yanaendelea kuongezeka kwa idadi na ukubwa ambapo yanasababisha vifo na upotevu wa mali. Hatari hii inachangiwa zaidi na kuwa sekta nyingi za kijamii

na kiuchumi hususan ya kilimo na usalama wa chakula hutegemea mvua.

Katika kukabiliana na changamoto na athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa nchi yetu, Mamlaka ya Hali ya Hewa ina jukumu la kuhudumia wadau na jamii kwa ujumla kwa kuzingatia mahitaji yao mahsusi. Ili Mamlaka iweze kukamilisha majukumu haya ni muhimu ikaongeza nguvu na kuwekeza zaidi katika kufanya uangazi, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kwa wakati kwa wadau wa sekta mbalimbali. Aidha tafiti mbalimbali zinazohusiana na hali ya hewa kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma za hali ya hewa kwa jamii lazima ziendeleo. Masuala haya yote yameainishwa katika mpango huu.

## **Ndugu Wanawarsha, Mabibi na Mabwana,**

Kama nilivyotangulia kusema kuwa lengo kuu la warsha hii ni kuongeza ufahamu (awareness raising) kwa wafanyakazi wa Mamlaka kuhusu rasimu ya Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ambao unatoa mwongozo wa kuendelea kuimarisha utoaji na utumiaji wa huduma bora za hali ya hewa katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Majadiliano na mapendekezo yenu juu yatasaidia kuweka mipango mizuri ya utekelezaji wake kwani sisi ndio wadau wakuu. Mpango huu utasaidia kuongeza wigo na ufanisi katika shughuli za Uangazi, na usambazaji wa taarifa za hali ya Hewa na hivyo kuchangia katika kuboresha kilimo, usalama wa chakula, afya na huduma nyingine zinazotegemea hali ya hewa.

## **Ndugu Wanawarsha, Mabibi na Mabwana,**

Napenda kuhitimisha hotuba hii fupi kwa kuwakaribisha washiriki wote katika warsha hii muhimu kwa kuboresha huduma zetu. Uelewa na majadiliano yenu ni muhimu sana ili tuweze kufaninkisha malengo ya warsha na malengo ya Mpango huu. Napenda pia kutoa shukrani kwa wataalamu wote walioshiriki kuandaa andiko hii.

Baada ya maneno haya machache napenda sasa kutamka kuwa warsha hii ya siku moja inayohusu kuongeza ufahamu kwa wafanyakazi wa Mamlaka kuhusu Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imefunguliwa rasmi.

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA***